UCHAGUZI MKUU 2005
Uandikishaji katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Waanza

• NEC yawahimiza wana-CCM, Wakereketwa na wananchi kujiandikisha.

Zoezi la kuandikisha Wapiga Kura kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambalo litaanza kutumika katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika Oktoba, 2005 limekwishaanza.

Kwa kuzingatia Ratiba iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wananchi waliokwisha jiandikisha ni wa mikoa ya Kanda ya Kusini (Lindi na Mtwara) na wale wa Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Ruvuma, Iringa, Rukwa na Mbeya).

Wananchi wa Kanda zilizobaki watajiandikisha kama ifuatavyo kwa kuzingatia Ratiba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi:

1. KANDA YA KATI (Mikoa ya Dodoma, Singida, Kigoma na Tabora) kuanzia tarehe 5 Desemba, 2004 hadi 25 Desemba, 2004.

2. KANDA YA ZIWA (Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara) kuanzia tarehe 12 Januari, 2005 hadi tarehe 1 Februari, 2005.

3. KANDA YA KASKAZINI (Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Manyara na Arusha) kuanzia tarehe 19 Februari, 2005 hadi 11 Machi, 2005.

4. KANDA YA PWANI (Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro) kuanzia tarehe 29 Machi, 2005 hadi 18 Aprili, 2005.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imetangaza kwamba uandikishaji kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utaendeshwa kwa kipindi cha siku 21 kwa kila Kanda isipokuwa Zanzibar. Vituo vitafunguliwa kila siku saa 2.00 asubuhi na kufungwa saa 12 jioni.

Ratiba ya kuandikisha wapiga kura wa Zanzibar wenye sifa ya kumpigia kura Rais wa Jamhuri ya Muungano tu itatolewa baadaye na Tume.

Sifa za Kuandikishwa

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 Ibara ya 5(1), na Vifungu 10(1) na 10(2) vya Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya 1985 na kifungu cha 15(1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani Na. 4 ya 1979 zimeainisha sifa zifuatazo za kuandikishwa kuwa Mpiga Kura:

- Kuwa raia wa Tanzania na;
- Kuwa na umri wa miaka 18 au zaidi au;
- Kuwa na umri wa miaka 18 au zaidi itakapofika siku ya uchaguzi.

Kukosa sifa za kuandikishwa

Kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Uchaguzi mtu anakosa sifa za kuandikishwa iwapo:

- Ana uraia wa nchi nyingine au;
- Ana ugonjwa wa akili au;
- Amehukumiwa kifo na Mahakama au;
- Anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita au;
- Amezuiliwa na Sheria kujiandikisha kuwa Mpiga Kura

Uandikishaji kituoni:

Kila mtu anayetaka kujiandikisha Kupiga Kura atakwenda kujiandikisha kwenye kituo kilicho karibu naye katika Kata anayoishi kwa kuzingatia yafuatayo:-

1. Mtu anayetaka kuandikishwa hana budi kujitambulisha kwa Mwandishi Msaidizi Na. 1 na kuomba kujiandikisha kwenye kituo rasmi cha kuandikisha.

2. Mwandishi Msaidizi Na. 1 akiridhika kwamba mwombaji ana sifa atamwelekeza anayeomba kujiandikisha, kwenda kupigwa picha mbili bila ya malipo hapo hapo kituoni.

3. Mwandishi Msaidizi Na. 1 atajaza kikamilifu Fomu Na. 1 sehemu A na Kadi ya Mpiga Kura na kuzisaini.

4. Mtu aliyeandikishwa ataweka saini kwenye Fomu Na. 1 sehemu A na B. Aidha ataweka saini au alama ya dole gumba la mkono wa kulia kwenye Kadi ya Mpiga Kura.

5. Mtu aliyeandikishwa ataweka alama ya Dole Gumba la mkono wa kulia kwenye Fomu Na. 1 Sehemu A na B.

6. Mwandishi Msaidizi Na. 1 atabandika picha moja kwenye Fomu Na. 1 sehemu B.

7. Mwandishi Msaidizi Na. 2 atabandika picha ya Mpiga Kura kwenye Kadi ya Mpiga Kura na kutengeneza kadi hiyo (Lamination).

8. Mwandishi Msaidizi Na. 2 atamkabidhi Kadi Mpiga Kura anayehusika na kumsisitizia kwamba aitunze vizuri.

9. Kwa mwombaji asiye na sifa, Mwandishi Msaidizi Na. 1 atakataa kumwandikisha na kumweleza sifa aliyokosa/alizokosa. Iwapo mtu huyo hajaridhika, Mwandishi Msaidizi ajaze Fomu Na. 3 na kumkabidhi mtu huyo ili, akipenda, aende kwa Afisa Mwandikishaji au Afisa Mwandikishaji Msaidizi.

10. Baada ya uandikishaji kwa siku

kukamilika Mwandishi Msaidizi Na. 1 ajaze Fomu Na. 2 (Batch Header) kuonyesha idadi ya Fomu zilizojazwa kwa siku hiyo. Fomu Na. 1 zilizojazwa sehemu A na B pamoja na Batch Header ziwekwe kwenye Bahasha Na. 8, bahasha ya kuhifadhia fomu zilizotumika kwa siku ataziweka kwenye Boksi.

Fomu Na. 2 (Batch Header) ijazwe kila siku hata siku ambayo hakuandikishwa mtu ye yote katika kituo na iwekwe kwenye Bahasha Na. 8.

11. Afisa Mwandikishaji atoe Taarifa ya Uandikishaji ya kila wiki kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Taarifa hii ionyeshe idadi ya walioandikishwa kwenye kila Kata na Jimbo.

Baada ya kukamilika uandikishaji wapiga kura

Tume, kwa mujibu wa kifungu cha 11A (1) cha Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya 1985 na kifungu cha 15A (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani Na. 4 ya 1979, itaandaa Daftari la Awali la Wapiga Kura. Daftari hili litakuwa na majina na picha za Wapiga Kura wote waliojiandikisha nchi nzima.

Kupokea Daftari la Awali

Afisa Mwandikishaji atapokea kutoka Tume Daftari la Awali kwa kila Kata ya Halmashauri. Atahakiki majina ya wapiga kura waliomo kwenye Daftari la Awali kwa kulinganisha na majina yaliyomo kwenye Fomu Na. 1 sehemu A.

Kufikisha Daftari la Awali kwenye Kata

Afisa Mwandikishaji atakabidhi Daftari la Awali la kila Kata kwa Afisa Mwandikishaji Msaidizi wa Kata inayohusika.

Kuweka mahali pa wazi na kukagua Daftari la Awali la Wapiga Kura

Afisa Mwandikishaji atatangaza kipindi cha kukagua Daftari la Awali kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya 1985, kifungu cha 22(1) na Sheria ya uchaguzi wa Madiwani Na. 4 ya 1979 kifungu cha 28(1).

Kwa mujibu wa kifungu cha 22(2) cha Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya 1985 na Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani Na. 4 ya 1979 kifungu cha 28(2). Afisa Mwandikishaji ataweka mahali pa wazi Daftari la Awali kwa kukaguliwa na kila mtu kwa muda wa siku saba.

Wakati wa kukagua Daftari la Awali kila Afisa Mwandikishaji Msaidizi wa Kata anatakiwa awemo katika ofisi ambapo Daftari limewekwa wazi. Kila Chama cha Siasa, chenye usajili kamili, kinaweza kuteua Mwakilishi atakayekuwepo katika ofisi hiyo.

Watu waliojiandikisha watakagua usahihi wa majina na taarifa zao. Iwapo haziko sahihi watatoa taarifa kwa Afisa Mwandikishaji/Afisa Mwandikishaji Msaidizi.

Utaratibu wa kuwasilisha pingamizi dhidi ya Uandikishwaji

Pingamizi linaweza kutolewa na mtu ye yote aliyeandikishwa kwa Afisa Mwandikishaji au Afisa Mwandikishaji Msaidizi, la kuondoa jina la mtu ye yote ndani ya Daftari la Awali kwa kujaza Fomu Na. 4 zilizoandaliwa na Tume. Kwa mujibu wa kifungu cha 24(1) cha Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya 1985, na kifungu cha 30(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani Na. 4 ya 1979, pingamizi linaweza kuwa la kuomba jina la mtoa pingamizi, au la mtu anayepingwa, kufutwa katika Daftari la Awali la Wapiga Kura. Watu wengine wanaoruhusiwa kutoa pingamizi ni Mkurugenzi wa Uchaguzi na Afisa Mwandikishaji.

Utaratibu wa kutoa uamuzi dhidi ya pingamizi

1. Iwapo sababu ya pingamizi ni kufariki kwa mtu anayepingwa, Afisa Mwandikishaji au Afisa Mwandikishaji Msaidizi amtake mtoa pingamizi kutoa uthibitisho wa madai yake au kujaza Fomu Na. 5B ili kuthibitisha kufariki kwa mpiga kura. Mtoa pingamizi akikataa kuthibitisha au kujaza Fomu hiyo madai yake yasizingatiwe.

2. Iwapo sababu ya pingamizi ni kukosa sifa kwa mtu anayepingwa, Afisa Mwandikishaji au Afisa Mwandikishaji Msaidizi, anatakiwa, kwa mujibu wa kifungu cha 26(1) cha Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya 1985 na kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani Na. 4 ya 1979, kuchunguza tuhuma zilizotolewa na kutoa uamuzi.

3. Kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi, mtu anayepingwa apewe taarifa ya maandishi ya pingamizi lililotolewa na kutakiwa kutoa utetezi wake baada ya siku saba tangu tarehe aliyotaarifiwa.

4. Kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi na kanuni za uandikishaji wa Wapiga Kura, Afisa Mwandikishaji au Afisa Mwandikishaji Msaidizi atoe uamuzi wa kukubali au kukataa pingamizi alilolifanyia uchunguzi ndani ya siku saba tangu alipotoa taarifa kwa anayepingwa.

   Uchunguzi hauna budi kufanywa mahali pa wazi ambapo mtoa pingamizi na anayepingwa watatoa hoja zao mbele ya Afisa Mwandikishaji au Afisa Mwandikishaji Msaidizi.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imevitaka vyama vya siasa kuzingatia na kuwaelimisha wanachama na wapenzi wao kwamba watu watakaojiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ndio watakaokuwa na haki kisheria ya kupiga kura katika Uchaguzi ujao wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Imesisitizwa kwamba hakutokuwepo na uandikishaji wa wapiga kura tena katika Uchaguzi Mkuu ujao baada ya Ratiba hii iliyopangwa na Tume.

Kwa kuzingatia zoezi hili la kisheria kikao cha NEC cha tarehe 25-26 Agosti, 2004 kilizingatia umuhimu wa Daftari hilo la Kudumu la Wapiga Kura na kuwataka Viongozi na Watendaji wote ndani ya Chama Cha Mapinduzi kuwahimiza wanachama, wakereketwa na wananchi wote kujiandikisha ili waweze kuwa na haki ya kisheria ya kupiga kura. ■